REPUBLIC OF KENYA

PROBATION AND AFTERCARE SERVICE KENYA

PACS

OFFENDERS CAN CHANGE

# MAUDHUI YA AZIMIO LA HUDUMA KWA WATEJA

Ahadi ya Heshima na Ubora katika Kutoa Huduma

@ The Probation and Aftercare Service, 2024
Haki zote zimehifadhiwa. Hati hii, au sehemu yake yoyote, haiwezi kunakiliwa tena au kutumiwa kwa njia yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Huduma ya Marejeleo na Huduma ya Baadaye.

Taifa Road, Reinsurance Plaza, Gorofa ya 11
S. L. Posta 42335-00100
Nairobi, Kenya
Barua Pepe: information@probation.go.ke
www.probation.go.ke

# Utangulizi

Idara ya Probesheni (PACS) ina jukumu kubwa katika ushughulikiaji wa makosa ya jinai kupitia utoaji wa ripoti mbalimbali za ushauri zinazosaidia mahakama na mamlaka nyingine za kutoa adhabu kufanya maamuzi mazuri zaidi kuhusu masuala ya dhamana, adhabu na kutolewa kifungoni wakati huo huo ikifanikisha na kuhakikisha usalama wa wahasiriwa na jamii.

Aidha, Huduma inahakikisha afua zinazotokana na ushahidi zinatolewa kwa wakosaji waliowekwa chini ya usimamizi mbalimbali wa kisheria kwa lengo la kuwarekebisha na kuwarejesha kwenye jumuiya na hivyo kupunguza kurudi katika uhalifu na kuwa na mabadiliko chanya ya kitabia. Idara ya Probesheni (PACS) inashirikiana kwa karibu na mashirika mengine ya kushughulikia jinai katika kutoa adhabu ya makosa ya jinai.

Majukumu makuu ya PACS katika kushughulikia utendaji haki katika makosa ya jinai ni haya:

1. Kutafuta taarifa kwa ajili ya utoaji haki kwenye makosa ya jinai.
2. Kusimamia amri za mahakama, adhabu na kurekebisha wakosaji na waliowahi kuwa wakosaji.
3. Kuwarejesha na kuwaanzishia maisha mapya wakosaji .
4. Kushiriki katika kuzuia uhalifu na usalama wa jamii.
5. Kuendeleza, kuhamisha na kushiriki katika kulinda haki za wahasiriwa na ustawi wao.

# Azimo

Azimio hili linaelezea majukumu muhimu ya Idara ya Probesheni na linaweka viwango vya utendaji na ahadi yetu ya heshima na ubora katika kutoa huduma.

Azimio pia linaangazia haki za wateja, wajibu na utaratibu wa malalamiko. Idara ya Probesheni inalenga kufanikisha utoaji wa haki, ulinzi na usalama wa jamii.

# Kusudi la Azimo hili

Azimio hili linalenga:

- Kukuza ufahamu wa aina ya huduma tunazotoa.
- Kuelezea viwango vya huduma ambavyo wateja wetu watarajie kuvipata.
- Kuainisha haki na upendeleo wa wateja wetu.
- Kuelezea utaratibu wa malalamiko na mrejesho.

# Dhima

**Dira**
Kuwa na jamii ya haki, salama, yenye ulinzi na isiyokuwa na uhalifu.

**Dhima**
Kukuza na kuimarisha utoaji haki, usalama wa jumuiya na ulinzi wa umma kwa kutoa ripoti za tafiti za kijamii, usimamizi, urekebishaji na urejeshaji katika jamii wa wakosaji wanaotumikia kifungo cha nje, msaada kwa wahasiriwa na uzuiaji wa jinai kutokana na sababu za kiuchumi na kijamii.

**Maadili**
- Usawa
- Kutegemeka
- Kuheshimu utu
- Usiri
- Uadilifu
- Weledi
- Mamlaka

# Mamlaka

**Mamlaka**

Tunapata mamlaka yetu kutoka kwenye Katiba, sheria, sera na mikataba ya kimataifa inayotoa miongozo ya kazi ya probesheni na urekebishaji wa wakosaji na waliowahi kuwa wakosaji wanaotumikia kifungo cha nje.

Kwa kazi hiyo, tunatoa ripoti za tafiti za kijamii kuhusu wakosaji mahakamani na mamlaka nyingine kwa madhumuni ya kutoa dhamana na masharti ya kujidhamini na utaratibu wa kufikia uamuzi wa kutoa adhabu na kuachiwa kutoka kifungoni kwa wakosaji; na kusimamia, kuwaanzishia maisha mapya, kuwarejesha kwenye jamii na kurekebisha wakosaji wanaotumikia vifungo mbalimbali vya nje katika jumuiya. Pia tunafanya kazi na wahasiriwa katika mchakato huu na kujitahidi kuepusha jinai na kutenda uhalifu tena.

**Tamko la Kusudi**

Tumedhamiria kuona haki inatendeka kulingana na sheria, usalama wa taifa na amani katika jamii.

**Wigo**

Huduma zetu zinapatikana katika ofisi za Probesheni zilizoko nchi nzima, katika majimbo yote, kila kaunti na kaunti ndogo.

# Tunachokifanya

- Kufanya tafiti za kijamii kuhusu washitakiwa, wakosaji na ni waombaji mahakamani kwa ajili ya kuandaa maelezo ya kuomba dhamana, taarifa za kesi kutajwa, kabla ya adhabu na baada ya adhabu

- Kuandaa na kutoa ripoti mahakamani na vyombo vingine vya kisheria kwa ajili ya utaratibu wa kufikia uamuzi na utoaji haki

- Kusimamia wakosaji na waliowahi kuwa wakosaji wanaotumikia vifungo vya nje, amri za kutolewa kifungoni na wale walioachiwa kwa msamaha wa rais

- Kuandaa na kutekeleza mipango ya kurekebisha wakosaji na waliowahi kuwa wakosaji wanaotumikia vifungo mbalimbali vya nje

- Kuwarejesha kwenye jamii na kuwaanzishia makazi upya wakosaji wanaotumkia kifungo cha nje na wale wanaotoka magerezani na kurudi uraian.

- Kuwezesha utaratibu mbadala wa kusuluhisha mizozo

- Kutoa huduma kwa ajili ya kulinda na kuendeleza haki na ustawi wa wahasiriwa na wakosaji na waliowahi kuwa wakosaji

- Kutoa makazi ya muda kwa wakosaji wenye uhitaji na kustahili na waliowahi kuwa wakosaji katika hosteli za probesheni na nyumba za mpito

- Kukuza shughuli za kuzuia jinai ili kuimarisha usalama wa jamii

# Utoaji Ripoti ya Utafiti wa Kijamii

| No. | Service | Requirements to Obtain Service | Cost | Timeline |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ripoti ya Maelezo ya Dhamana | Amri ya Mahakama inayotaka kuwasilisha Ripoti ya Maelezo ya Dhamana | Bure | Siku 14 (Utapewa sababu za kuridhisha endapo itachukua muda mrefu zaidi) |
| 2 | Ripoti ya Afisa wa Probesheni | Amri ya Mahakama inayotaka kuwasilisha Ripoti ya Afisa wa Probesheni | Bure | Siku 14 (Utapewa sababu za kuridhisha endapo itachukua muda mrefu zaidi) |
| 3 | Ripoti ya Afisa wa Huduma za Jumuiya | Amri ya Mahakama inayotaka kuwasilisha Ripoti ya Afisa wa Huduma za Jumuiya | Bure | Siku 14 (Utapewa sababu za kuridhisha endapo itachukua muda mrefu zaidi) |
| 4 | Ripoti ya Mapitio ya hukumu | Amri ya Mahakama inayotaka kuwasilisha Ripoti ya Mapitio ya hukumu | Bure | Siku 14 (Utapewa sababu za kuridhisha endapo itachukua muda mrefu zaidi) |
| 5 | Ripoti ya athari aliyopata Mhasiriwa | Amri ya Mahakama inayotaka kuwasilisha Ripoti ya athari aliyopata Mhasiriwa kwa mahakama | Bure | Siku 14 (Utapewa sababu za kuridhisha endapo itachukua muda mrefu zaidi) |
| 6 | Ripoti za Kabla ya kuachiwa wakosaji | Ombi kutoka Kamati ya Msamaha na Ushauri | Bure | Siku 30 (Utapewa sababu za kuridhisha endapo itachukua muda mrefu zaidi) |
| 7 | Ripoti za Urekebishaji Mazingira | Ombi kutoka Hosteli ya Probesheni, Bodi ya Wageni ya Jela ya Watoto, Shule ya Mafunzo | Bure | Siku 30 (Utapewa sababu za kuridhisha endapo itachukua muda mrefu zaidi) |

# Uongozi wa Wakosaji katika Jumuiya

| No. | Service | Requirements to Obtain Service | Cost | Timeline |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kupelekwa Hosteli za Probesheni | Amri ya mahakama inayomtaka mkosaji kupelekwa Hosteli za Probesheni | Bure | Siku 30 (Utapewa sababu za kuridhisha endapo itachukua muda mrefu zaidi) |
| 2 | Kufanya tathmini ya wakosaji au waliowahi kuwa wakosaji | Kwenye jumuiya, Waraka wa Rais wa Kuachiwa, Wafungwa, Leseni ya Bodi ya Wageni, Waraka wa Bodi ya Kuachiwa Wafungwa | Bure | Tathmini inafanyika katika hatua na vipindi mbalimbali wakati mkosaji akiwa chini ya usimamizi |
| 3 | Amri ya mahakama ya usimamizi wa wakosaji na waliowahi kuwa wakosaji | Kwenye jumuiya, Waraka wa Rais wa Kuachiwa, Wafungwa, Leseni ya Bodi ya Wageni, Waraka wa Bodi ya Kuachiwa Wafungwa | Bure | Kwa kipindi cha uhalali wa amri ya mahakama au Waraka wa Rais wa Kuachiwa Wafungwa au Leseni ya Bodi ya Wageni au Waraka wa Bodi ya Kuachiwa Wafungwa |
| 4 | Amri ya mahakama ya urekebishaji na namna ya kuwatendea wakosaji au waliowahi kuwa wakosaji | Kwenye jumuiya, Waraka wa Rais wa Kuachiwa, Wafungwa, Leseni ya Bodi ya Wageni, Waraka wa Bodi ya Kuachiwa Wafungwa | Bure | Kwa kipindi cha uhalali wa amri ya mahakama au Waraka wa Rais wa Kuachiwa Wafungwa au Leseni ya Bodi ya Wageni au Waraka wa Bodi ya Kuachiwa Wafungwa |
| 5 | Amri ya mahakama ya kuwapatia makazi mapya na kuwarejesha wakosaji na waliowahi kuwa wakosaji | Kwenye jumuiya, Waraka wa Rais wa Kuachiwa, Wafungwa, Leseni ya Bodi ya Wageni, Waraka wa Bodi ya Kuachiwa Wafungwa | Bure | Kwa kipindi cha uhalali wa amri ya mahakama au Waraka wa Rais wa Kuachiwa Wafungwa au Leseni ya Bodi ya Wageni au Waraka wa Bodi ya Kuachiwa Wafungwa |

# Haki zako kama Mteja wetu

Unapokuwa ukishughulikiwa nasi, unayo haki ya:

- Kutendewa kwa haki, heshima na utu bila ya kuwa na aina yoyote ile ya ubaguzi.
- Kuelezwa na kuwasiliana katika lugha unayoielewa vizuri zaidi.
- Kupewa maelezo kuhusu amri zote zilizotolewa ambazo zinaweza kukuathiri.
- Kutunza siri ya maelezo yote binafsi isipokuwa tu kama wewe au mahakama itatoa idhini siri zako kuwekwa wazi.
- Kupata habari inayokuhusu isipokuwa tu kama imekatazwa kisheria.
- Kutaka kupewa utambulisho na kusudi la kutembelewa kokote na Afisa wa Probesheni.
- Kutafuta mabadiliko ya amri zozote zilizoidhinishwa ambazo zinaweza kukuathiri.
- Kutafuta huduma ya wakili au ushauri.

# Wajibu wako kama Mteja wetu

Ili kukutumikia vyema, tunatarajia kwamba:

- Utawakubali na kuwatendea wafanyakazi wetu kwa heshima na weledi na hutatenda kwa namna isiyokuwa adilifu.
- Utatupatia kwa haraka, usahihi, kwa uaminifu na kwa wakati maelezo kwa ajili ya haki kutendeka.
- Unafuata sheria zozote zilizopo, kanuni na taratibu zinazosimamia huduma tunazotoa.
- Utatupatia mrejesho kuhusu huduma zetu.

# Kushughulikia malalamiko yako

Ili kutoa malalamiko yako kuhusu huduma ambazo hazikukuridhisha, unaweza kutoa malalamiko yako wewe mwenyewe, au kwa kupiga simu, kwa maandishi na kwa barua pepe. Tunazo ngazi mbalimbali ambazo unaweza kutoa malalamiko yako:

- Afisa wa Probesheni anayeshughulikia suala lako au Afisa wa Probesheni mwingine yeyote.
- Afisa Mkuu wa Kituo cha Probesheni.
- Mkurugenzi wa Probesheni wa Kaunti.
- Mratibu wa Jimbo wa Huduma ya Probesheni.
- Mkurugenzi wa Huduma za Probesheni.
- Katibu Mkuu anayehusika na Maadili na Tume ya Kupambana na Rushwa, Tume ya Uongozi wa Sheria, au mamlaka nyingine yoyote.

Unaweza pia kutumia kadi yetu ya taarifa ya raia, visanduku vya malalamiko na maoni, madawati ya malalamiko/ huduma kwa wateja, fomu ya mrejesho kwenye tovuti yetu. Tegemea hatua za haraka katika kushughulikia malalamiko yako kwenye yoyote ya hizo ngazi hapo juu.

*Ilani ya Kujitoa hatiani: Tunafungwa na sheria husika, sera za serikali, taratibu na kanuni zinazoeleza jinsi tunavyofanya kazi, namna tunavyoshugulikia malalamiko na maamuzi tunayofanya. Ingawa tunaweza kubadilisha namna tunavyotoa huduma, hatuna mamlaka ya kubadilisha maamuzi yaliyotolewa na mahakama au malalamiko yaliyo nje ya mamlaka yetu.*

# JINSI YA KUTUFIKIA

The Probation and Aftercare Service Headquarters
Taifa Road/ Aga Khan Walk, Reinsurance Plaza Building, Gorofa ya 11
S. L. Posta 42335-00100 Nairobi, Kenya

**Simu**.: +254-020-2652335 /3311303 /2215658 /2240057 /2224016
**Rununu**.: +254-722-104621/1044626

**Tovuti**: www.probation.go.ke
**Barua Pepe**: information@probation.go.ke

Twitter/ Facebook/ LinkedIn/ Youtube: @ProbationKE
WhatsApp: 0759-603-921